**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Juni, 2015.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013*

---

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda dhidi ya hila na mbinu za maadui zangu za kutaka kudhoofisha harakati zangu za ukombozi wa taifa hili, na kunipa nguvu na maarifa zaidi ya kusonga mbele. Pili napenda kuwashukuru Makamanda wote wa CHADEMA kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA Taifa (BAWACHA). Napenda kukiahidi chama changa CHADEMA, na wananchi wote wapenda mageuzi kwamba, nitaitumikia nafasi hii ya uenyekiti wa BAWACHA Taifa kwa uadilifu mkubwa na kwa moyo wangu wote.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru sana wapiga kura wangu – wananchi wa Kawe kwa imani kubwa walioonesha kwangu na kwa ushirikiano mzuri wanaoendelea kunipa katika kazi zangu za kibunge na kijamii. Kupitia kwao nimeingia katika ramani ya Tanzania na kupitia kwao pia nimeingia katika ramani ya Dunia. Ni matumaini yangu kwamba

iwapo chama changu kitaniteua kuwania tena Ubunge katika Jimbo hilo, hamtaniangusha. Ombi langu kwenu na kwa wananchi wote wa Dar es Salaam, mjitokeze kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Wapiga kura pindi litakapopita huko kwa kuwa Taifa zima linawategemea wananchi wa Dar es Salaam kuongoza mabadiliko. Hivyo makamanda wa Dare es Salaam, naomba tukaze buti tusije tukatia aibu katika uchaguzi wa Oktoba, 2015.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa uhai wa Bunge hili la Kumi unaelekea ukiongoni, hii itakuwa ni hotuba yangu ya mwisho katika Bunge hili nikiwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hata hivyo, namalizia muda wangu wa utumishi nikiwa na furaha kubwa kwani kwa muda wote wa miaka mitano ya uhai wa Bunge hili niliitendea haki nafasi yangu ya Waziri Kivuli wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nadhani watanzania waliona jinsi Kivuli changu kilivyomfunika aliyekuwa Waziri mwenye dhamana wakati huo Mhe. Profesa Anna Tibaijuka.

**Mheshimiwa Spika,** namalizia utangulizi wangu kwa kuwasihi wananchi wote kutumia fursa hii ya maboresho ya Daftari la Wapiga Kura, kujiandikisha na kutumia haki yao ya kidemokrasia ipasavyo ili kuwachagua madiwani, wabunge na Rais watakaopendekezwa na UKAWA, ili kuuondoa utawala wa CCM ambao umewafanya watanzania kuwa masikini kwa miaka yote 53 ya uhuru.

## 2. TATHIMINI YA KAZI ZA UPINZANI KATIKA WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MIAKA MITANO ILIYOPITA (2010 – 2015).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itakumbukwa kwa kazi nzuri ya

kutoa mawazo na fikra mbadala kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa majukumu yaliyopo chini ya Wizara hii. Hata hivyo, kutokana na ugumu wa Serikali hii ya CCM wa kukiri udhaifu, ilibeza sana ushauri mzuri wa Kambi Rasmi ya Upinzani uliofanyiwa utafiti na hivyo kuacha mambo mengi kuendelea kuwa hovyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itakumbukwa kwa kuibua kasoro na matatizo mengi chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa lengo la kuitaka Serikali ambayo kimsingi ndiyo yenye dhamana na yenye mamlaka ya kukusanya kodi za watanzania itatue kasoro na matatizo hayo ili wananchi waweze kunufaika na rasilimali ardhi yao na kuishi kwenye nyumba zenye staha kwa mustakablali mwema wa maisha yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa faida ya wananchi na wahanga wa migogoro ya ardhi, napenda kuchukua fursa hii kutaja baadhi ya masuala muhimu kuhusu ardhi nyumba na maendeleo ya makazi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliyaibua na kutaka yashughulikiwe na Serikali:

i. Kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilikemea na kulaani uporaji na ugawaji holela wa ardhi ya watanzania kwa mataifa ya nje chini ya usimamizi wa Serikali kwa hila au kisingizio cha uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliibua jambo hili kutokana na taarifa za kitafiti zilizofanywa na taasisi ya hapa nchini ya HAKIARDHI ambayo pamoja na mambo mengine imeonyesha kwamba kati ya migogoro ya Ardhi, **1,825** iliyoripotiwa mwaka 2011, migogoro **1,095** ilikuwa inahusu

wawekezaji wakubwa[1]. Halikadhalika, tafiti zilizofanywa hivi karibuni na taasisi za kimataifa zikiongozwa na ***'The International Land Coalition (ILC)'***[2] zinazo-onyesha kwamba kuna mikataba mikubwa zaidi ya **1,217** ya utoaji ardhi kwa masuala ya kilimo takriban hekta milioni **83.2**[3] imeridhiwa au iko katika mchakato wa kuridhiwa kati ya mwaka 2007-2012.

**Mheshimiwa Spika,** Bara la Afrika ambalo ndio mlengwa mkuu wa mkakati huu wa uporaji wa ardhi linaongoza kwa kuwa na "mikataba" **754** inayojumuisha eneo lenye ukubwa wa hekta milioni **56.6**[4]**,** ikifuatiwa na Bara la Asia lenye hekta **17.7** milioni, huku Bara la Amerika ya kusini likishika nafasi ya tatu kwa kujumuisha ardhi yenye ukubwa wa hekta milioni **7.**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 ambazo zinaongoza kwa kupokea maombi mengi zaidi ya 'wawekezaji'[5]. Nchi nyingine ni Sudan, Ethiopia, Msumbiji , Madagascar, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Katika Bara la Asia[6] nchi zinazoongoza ni Philippines, Indonesia na Laos[7].

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwenendo huo wa uporaji wa ardhi unaoendelea duniani na hapa nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuchukua tahadhari

---

[1] DILAPS POLICY Brief No:9 2013

[2] The International Land Coalition ( ILC), The centre for Development and Environment (CDE), CIRAD, The GIGA German Institute of Global and Area studies na The Deutshe Gesellschaft fur Internationale Zusammenarbeit (GIZ)

[3] Kiasi hicho ni sawa na 1.7% ya ardhi yote ya dunia inayofaa kwa kilimo

[4] Inakadiriwa ardhi husika ni sawa na 4.8% ya ardhi yote inayofaa kwa kilimo afrika au ukubwa husika ni sawa na Nchi ya Kenya

[5] Mataifa mengine yameshaingia mkataba na wengine wako katika hatua za awali za kuingia mikataba

[6] Transnational Land Deals for Agriculture in the Global South, Analytical Report based on the Land Matrix Database, Ward Anseeuw and Matheau Boche et al, 2012

[7] According to the anti-corruption non-governmental organization Transparency International, Laos remains one of the most corrupt countries in the world

mapema kuilinda Ardhi ya Tanzani isije ikachukuliwa na wageni na watanzania wakabaki kama watumwa ndani ya nchi yao. Katika kufanya hivyo, tunaitaka Serikali kurejea maneno ya Baba wa Taifa aliyesema mwaka 1958 kwamba: nanukuu, *" Nchi kama yetu , ambayo waafrika ni masikini na wageni ni matajiri, kuna uwezekano kwamba mwafrika akiruhusiwa kuiuza ardhi, katika miaka ya themanini au miaka ijayo, ardhi ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri wageni, na wenyeji watakuwa watwana. Lakini hata kama wageni wasingekuwa matajiri, litaibuka tabaka la watanganyika matajiri wajanja. Tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu, katika muda mchache, kutakuwa na kundi dogo waafrika watakaokuwa na ardhi na walio wengi watakuwa watwana''* Tunaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imechukua hatua gani za kuzuia uuzaji wa ardhi kwa wageni kiholela?

ii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilikemea na kupinga Ufisadi wa ardhi uliokuwa unafanywa na viongozi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi. Tulienda mbele Zaidi kuwataja vigogo hawa kwa majina na nyadhifa zao! Kama ilivyo ada hakuna hatua zozote zilizochukuliwa!,hali inayopelekea mwendelezo wa kadhia hii kama itakavyobainishwa baadaye katika hotuba hii'.

iii. **Mheshimiwa Spika,** kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani pia ilibaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria namba 5 ya ardhi ya vijiji ambapo viongozi wa Serikali walikuwa wakigawa ardhi kiholela bila kuzingatia matakwa ya sheria hizo, jambo ambalo lilikuwa ni chimbuko la migogoro mingi ya ardhi katika vijiji vingi. 'Hakuna hatua zilizochukuliwa, viongozi wa vijiji wanaendelea kugawa

ardhi kwa wawekezaji kinyume na utaratibu kama ambavyo tutaainisha hapo baadaye'!

iv. Kambi ya upinzani ilihoji juu ya mradi wa viwanja 20,000 , mradi ambao ulitawaliwa na wizi,ufisadi na udanganyifu mkubwa!(Mradi huu ulifanyika kipindi ambacho Mama Salome Sijaona alipokuwa katibu Mkuu wa wizara ya ardhi)Viwanja vingi viliishia kwa watu wachache!!(watumishi wa wizara waliopewa mamlaka ya kusimamia Mradi) na kuelekeza ukaguzi maalum(Special Audit)ufanyike ili kujua nani ni wamiliki halisi!, mpaka sasa hakuna taarifa yoyote juu ya ukaguzi wa mradi husika, licha ya Kamati ya Bunge ya ardhi na Maliasili nayo kuhoji juu ya jambo hili. !!

v. Kambi rasmi ya upinzani ilihoji juu ya migogoro isiyo kwisha baina ya wizara ya maliasili na utalii na wanavijiji wanaoishi pembezoni mwa hifadhi. Hakuna hatua za maana zilizochukuliwa, tumeendelea kushuhudia malalamiko mazito ya wabunge wakati wakichangia hotuba ya maliasili na utalii.

vi. Kambi ya upinzani ilihoji juu ya uporaji ardhi wilaya ya Mafia kwa kile kinachoitwa uwekezaji (Tumaini Plantation Ltd). Zaidi ya Kaya 2500 za wananchi wa vitongoji vya Mikongoni, Mkamba, Kipora, Kifinge, Mlundo, Gonge, Chunguruma, Baleni, Minaki vilivyopo katika vijiji vya Kirongwe, Baleni, Jojo, Gonge, Kifinge na Ndagoni, wilayani Mafia, mkoani Pwani, ziko katika ***Msiba Mkuu*** wakisubiri kufukuzwa majumbani mwao kutokana na serikali kutaka kukabidhi maeneo yao ya asili kwa mwekezaji.

vii. Kwa miaka yote ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upizani Bungeni, iliitaka Serikali kushugulikia migogoro mikubwa ya

ardhi baina ya wakulima na wafugaji ambayo kwa nyakati tofauti imepelekea umwagaji damu miongoni mwa wananchi. Wakati migogoro hii inachochewa na uhaba wa ardhi,kuna genge la watu wachache wanahodhi maeneo makubwa ya ardhi, ambayo hayajaendelezwa (Mashamba pori), huku serikali ikiwa haina ujasiri wa kuyarejesha ili yatumike kwa manufaa ya watanzania walio wengi.

**Mheshimiwa Spika,** bado wakulima na wafugaji wanaendelea kuuana, hakuna hatua zozote za maana zilizochukuliwa, licha ya Bunge lako tukufu, kupitia Kamati teule ya Bunge kutoa taarifa ya chimbuko la migogoro husika!

viii. Kambi Rasmi ya Upinzani iliainisha matatizo makubwa katika tathmini ya malipo ya fidia kwa wananchi wanaotakiwa kuondoka katika maeneo yao kupisha matumizi mapya ya ardhi. Katika juhudi za kutatua tatizo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Seikali kulipa fidia stahiki kwa wananchi wanaotakiwa kuondoka katika maeneo yao kupisha matumizi mapya ya ardhi. Suala la fidia kwa wananchi bado ni donda ndugu!

ix. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilihoji juu kuendelea kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi jambo ambalo limesababisha wananchi kuendelea kuishi katika makazi duni na hivyo kuhatarisha usalama wao na kutweza utu wao. Licha ya Mbwembwe za Katibu Mkuu wa CCM ndugu Kinana, kudandia hoja ya Kambi ya upinzani, na kuahidi kuielekeza serikali ya Chama chake kulifanyia kazi, hakuna hatua za dhahiri zilizofanyika kuwapunguzia wananchi adha hii!

x. Kambi Rasmi ya Upinzani pia ilikemea na kupinga tabia mbaya ya Serikali na taasisi zake kutolipa kodi za pango kwa wakati kwa Shirika la Nyumba la Taifa na hivyo kulirudhisha nyuma kimaendeleo.

xi. Tuliitaka Serikali kubatilisha mkataba wa kifisadi kati Kampuni ya Uwindaji ya Game Frontiers of Tanzania Limited na Kampuni mbili za nje za uchimbaji madini za Uranium Resourses PLC na Western Metals, kufanya utafiti wa uchimbaji wa madini ya Uranium kwenye kitalu cha uwindaji katika kijiji cha Mbarang'andu kinyume cha sharia na kujipatia kipato isivyo halali. 'Hakuna la maana lililofanyika Zaidi ya kulindana'

xii. Tuliitaka Serikali kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Kodi za Nyumba (Real Estate Regulatory Authority) ili kuratibu, kuweka viwango na miongozo ya kodi za nyumba ili kuwaondolea wananchi wapangaji wa nyumba adha kubwa ya gharama kubwa za pango zisizo na viwango. Aidha, pendekezo hili lililenga pia kuipatia Serikali mapato makubwa kupitia sekta ya nyumba ambayo kwa sasa hayakusanywi ipasavyo.

xiii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliishauri serikali kusitisha ugawaji wa ardhi kwa wageni (kwa muda) hadi tathmini ya kina ifanyike. Ili kuweza kuwa na mpango thabiti wa matumizi bora ya ardhi! Ushauri huu ulipuuzwa!

xiv. Tulionesha pia jinsi Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba bora na Vifaa vya Ujenzi alivyoshindwa kuleta mabadiliko kutokana na kuongezeka kwa nyumba zisizo bora (kama vile nyumba za tembe, tope na nyasi) na kuongezeka kwa bei ya vifaa vya ujenzi.

xv. Tuliitaka Serikali kuweka ukomo wa ardhi ya kilimo kwa

wawekezaji.

xvi. Kambi ya Upinzani ilihoji juu ya utekeleza wa Taarifa ya Kamati (ya Lukuvi)- alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ambayo iliundwa tarehe 18 Juni, 2010 ikiwa na jukumu la kuchunguza maeneo ya wazi yaliyomo katika Jiji la Dar es salaam, ambayo yamevamiwa, kuendelezwa au kuuzwa kinyume na taratibu za mipango miji (Ripoti iko kwenye makabati imejaa vunmbi).

**xvii.** Kambi ya upinzani iliitaka Serikali kuleta Bungeni Taarifa ya uchunguzi ya kuanguka kwa magorofa Dar es salaam ya mwaka 2006 na hatua zilizochukuliwa na baada ya ukaguzi !Na nyumba ngapi zilitakiwa kuvunjwa. Halikadhalika tulitaka Ukaguzi ufanyike kwenye majengo yote yaliyojengwa na Ladha Construction LTD (aliyehusuka na ujenzi wa jengo, katika Mtaa Indira Ghandhi – Dar es Salaam, lililoanguka nakuua watu wasiopungua 21). Tuliiambia Serikali kuwa kuna maghorofa aliyoyajenga yenye wapangaji ndani yake na ziko kwenye mazingira hatarishi.

**Mheshimiwa Spika,** Mpaka sasa hakuna hatua zilizochukuliwa licha ya maagizo ya wizara ya ardhi kuitaka Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kubomoa (jengo la ghorofa 16) lililopo kwenye kiwanja Na 1662 kitalu 75 mtaa wa Idira Ghandi/Asia (Jengo pacha ya jengo lililoua watu wasiopungua 21) kupitia barua yenye kumbukumbu namba C.A 174/333/05/107 ya tarehe 5/04/2013. kwa kukiuka Mpango wa uendelezaji .

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya mbwembwe na matamko ya matambo ya viongozi wa Kitaifa,(Mkuu wa wilaya, Mkuu wa Mkoa , Waziri wa ardhi/ Ujenzi na hatimaye Rais wa

Jamuhuri ya Muungano), leo ni mwaka wa '2' jengo hilo halijabomolewa, na wala Halmashauri haijatoa notisi ya kumtaka mwenye jengo abomoe!.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kwamba; moja ya sababu zinazotolewa na Halmashauri na Wizara ni kwamba "wanazingatia maelekezo ya Katibu Mkuu Kiongozi (Ndugu Ombeni Sefue) aliyotoa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi ambayo aliwaagiza waepuke kufanya jambo ambalo litaisababisha serikali kufikishwa mahakamani!(Barua imeambatanishwa). Hakika huu utawala wa CCM ni kama wa Kambale (yani baba, mama na watoto, - wote wana ndevu). Inakuwaje Rais anaagiza,Katibu Mkuu Kiongozi anazuia?!!

**Mheshimiwa Spika,** inaonekana serikali ya CCM inasubiri watanzania wengine wafe ndio waamke kutoka katika lindi la usingizi !!

**Mheshimiwa Spika,** masuala ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeyafanya kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ni mengi na siwezi kuyataja yote hapa. Utekelezwaji wa ushauri na maoni ya Kambi ya upinzani umekuwa wa kiwango duni sana kwa kuwa waliopewa dhamana hawaoni umuhimu wa kuwajibika. Hali hii imepelekea marudio ya makosa yaleyale katika maeneo mengine ya nchi hii kwa kiwango kilekile.

## 3. VIGOGO WA CCM WANAVYOHUSIKA NA UPORAJI WA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** Kama ambavyo imekuwa ada, kila mwaka katika hotuba ya bajeti tumekuwa tukiliambia hili Bunge na watanzania kwa ujumla, juu ya ushiriki wa vigogo wa CCM na serikali katika kuchochea

au kuanzisha migogoro ya ardhi! (Rejea hotuba za kambi ya upinzani mwaka 2011/12, 2012/13 na 2014/15). Na kwa kuwa serikali hii ya CCM haina uthubutu wa kuchukua hatua, matukio mapya yanazidi kujitokeza na mwaka huu 2015/16 sakata la uporaji wa Ardhi linamhusisha Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, ndugu Leonidas Gama

**Mheshimiwa Spika,** Kiongozi huyu anaelezwa kuingia katika mkoa huo kwa mbwembwe nyingi akijipambanua kwamba anahitaji Halmashauri kutenga maeneo maalum ya uwekezaji! Halmashauri zikiamini kwamba kigogo huyu ana nia njema ya kuleta maendeleo zilipokea wito huo kwa mikono miwili! Moja kati ya Halmashauri hizo ni Halmashauri ya wilaya ya Rombo ambayo ilitwaa ardhi kutoka kwa wananchi na kuwalipa fidia ya jumla ya shilingi **milioni 168.**

Kada huyu wa CCM alikwenda China (kwa gharama za serikali) na kuja na watu wawili wanaoitwa 'wawekezaji' Katika hali ya kushangaza juu ya ardhi iliyolipwa fidia kwa fedha za umma ilianzishwa kampuni ya binafsi ya ***JUN YU INVESTMENT INTERNATIONAL COMPANY LTD***. Wanahisa katika kampuni husika ni Wang Zhigang – raia wa China (hisa 48,000), Feng Hu - raia wa China (hisa 49,000), na Muyanga Leonidas Gama – raia wa Tanzania (hisa 3,000). Huyu Muyanga Leonidas Gama ni mtoto wa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

**Mheshimiwa Spika,** tumeambatanisha nakala ya Memorandum of Association (MOA) husika kama sehemu ya hotuba hii! **(Tazama kielelezo na.1 na 2)**

**Mheshimiwa Spika**, Habari tulizonazo ni kwamba Mkuu wa Mkoa anamiliki hisa 20, 000 ambazo ni hisa 10,000 zilizofichwa kwa mwanahisa

wa kwanza na 10,000 nyingine kwa mwanahisa wa pili kwa mkataba wa 'siri uliofichwa'. **(Tazama kielelezo na. 3)** Katika hali ya kushangaza halmashauri ya Rombo ambayo iliwekeza fedha zake shilingi milioni 168 haitambuliwi na wala haina hisa hata moja katika Kampuni hiyo!

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za ki-inteligensia ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo; zinaonesha kwamba 'wawekezaji hao wa kichina' walilipa shilingi **milioni 500** kama fidia kwa wananchi katika ardhi hiyo hiyo (ambayo Halmashauri ya Rombo ilishalipa shilingi 168 milioni) - fedha ambayo mpaka sasa haijulikani iko wapi!!

**Mheshimiwa Spika,** Kama hiyo haitoshi; Kigogo huyu pia anahusisshwa na tuhuma za kutaka kufanya ufisadi katika eneo lililopo Kilacha (linalogusa jimbo la Vunjo na Rombo) lenye ukubwa wa hekta 2700. Eneo hili lilikuwa mali ya ushirika uliokuwa ukifahamika kwa jina la LOCOLOVA. Wananchi wanaishi na kufanya shughuli zao za kila siku!! Eneo hili linanyemelewa kwa udi na uvumba na kigogo huyu kwa kisingizio cha uwekezaji! Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba; mbinu alizozitumia katika uporaji wa ardhi ya Wananchi wa Rombo ndizo anazotarajia kuzitumia tena katika eneo hili!

**Mheshimiwa Spika,** Kada huyu wa CCM (ambaye ndiye mwakilishi wa Rais katika Mkoa huo) anatajwa tena katika mgogoro wa ardhi unaofukuta sasa hivi unaokihusisha kiwanja cha Mawenzi, chenye hati namba C.T 056035 kilichokuwa chini ya miliki ya ***The Registered Trustees of Mawenzi Sports Club.***[8] Kiwanja hiki kilikuwa na hatimiliki ya miaka 33 iliyokwisha mwaka 1974. Baada ya muda wa miliki ardhi kwisha

[8] Registered Trustees of India Sports Club ilipata certificate of incorporation mwaka 1950 tarehe 22 Desemba. Mwaka 1961 waliteua mdhamini mwingine baada ya mmojawapo kufariki; na kutaarifu Kabidhi wasii Mkuu. Tarehe 22 Desemba 1964 Registered Trustees of Indian Sports Club ilibadili jina na kuwa Registered Trustees of Mawenzi Sports Club ikiwa chini ya wadhamini iliyokuwa Indian Sports Club.

kisheria,na kufuatia mipango ya serikali ya kuendeleza mji wa Moshi mwaka 1994 , kupitia tangazo la serikali **No 606,** la 23/12/1994 -aliyekuwa waziri wa ardhi kipindi hicho Mhe. Edward Lowassa alitoa 'amri ya kutwaa' maeneo mbali mbali[9] likiwemo eneo lenye mgogoro.[10]

**Mheshimiwa Spika ,**

Kufuatia utwaaji wa eneo tajwa tarehe 12/4/2001 aliyekuwa waziri wa ardhi, Mhe. G.A Cheyo 'alitoa amri ya kuendeleza' mji wa Moshi, amri iliyochapishwa na tangazo la serikali no 112 la 15/6/2001 (eneo lenye mgogoro likiwa sehemu ya eneo husika). Pamoja na mambo mengine kifungu na.3 kimeweka wazi fursa ya pingamizi (ndani ya miezi miwili baada ya Tangazo kutolewa) kwa yeyote mwenye maslahi katika eneo husika! Hakuna pingamizi lolote lililowekwa!

**Mheshimiwa Spika,** Eneo husika lilikuwa salama chini ya wakuu wa mikoa wote waliopita, lakini hali ilibadilika alipoletwa bwana Gama, ambaye amekuwa akitumia ofisi yake kushinikiza kiwanja husika kukabidhiwa kwa genge la matapeli, ambao wametengeneza nyaraka feki na kuziwasilisha Rita na kisha kujitambulisha kama 'wadhamini wapya – 'Trustees' baada ya kukabidhiwa jukumu hilo na 'wadhamini wa awali'.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati 'matapeli' hawa wanaotambulika kwa majina 'Amratlal N. Pattn na Hittesh H.Solani wakionyesha kwamba kikao cha makabidhiano kilifanyika tarehe 5/1/2008 mbele ya uwepo wa 'wadhamini wa awali' ndugu Devchad Nathu Shah na Mohamedali Sharriff; taarifa za uhakika ambazo Kambi ya upinzani inazo, Ndugu Devchad Nathu Shah alishafariki dunia tangu mwaka 1979 , wakati Mohamed Shariff alifariki tangu mwaka 1998.

[9] The LandAcquisition Act , 1967 ( No 47 of 1967, made under section 34. Imetolewa na E.N Lowassa, waziri wa Ardhi , Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dar es salaam 21 / 10/1994

[10] Eneo husika liko kwenye mchoro wa mpango miji no 4/1473/691

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 26/11/2014 Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, akijibu dokezo lililowasilishwa kwake na Katibu Tawala Msaidizi kuhusiana na kiwanja tajwa hapo juu, anamwelekeza RAS aandike barua kwenda kwa Mkurugenzi wa Manispaa , na kumuonya asimzuie 'mwenye mali' kumiliki 'mali yake'![11]

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji:- inakuwaje wadhamini waliofariki mwaka 1979 na 1998 [12] wakae tena kwenye kikao cha Januari, 2008? Ikumbukwe huyu ndio mwakilishi wa Rais Kilimajnaro…halikadhalika Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa (Polisi na idara za usalama wa Taifa za mkoa zote ziko chini yake )! Na kubwa Zaidi ni mjumbe wa Kamati ya siasa ya chama cha Mapinduzi ya Mkoa!! Na kama hiyo haitoshi matapeli haya yakijua 'wadhamini' walishafariki toka mwaka 1979 na 1998; waliendelea kupeleka kumbukumbu za *'Returns of Trustees'* za miaka (2000-2008), zote zikiwa zimewasilishwa RITA kwa mkupuo mwaka 2012 zikiwa na saini za 'marehemu'!

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kazi njema iliyofanywa na Mkurugenzi Mkuu wa RITA aliyebatilisha uamuzi wake wa awali baada ya uongozi wa Moshi Manispaa kumpelekea nyaraka mbali mbali zilizoainisha udanganyifu husika,!! Hata hivyo tunatambua kuna mchakato unaoendelea wa kuwapatia 'matapeli'hawa hati mpya, na kwa kuwa kuna msukumo mkubwa wa Mkuu wa Mkoa 'ambaye anatuhumiwa kuvuta milioni 400' yawezekana mchakato husika ukafanikiwa au umeshafanikiwa!

---

[11] Nyaraka imeambatanishwa kama sehemu ya taarifa

[12] Marejesho ya taarifa za Trustees kwa Kabidhi wasii Mkuu ziliendelea kurejeshwa hadi tarehe 19/11/1965,wakati huo wakiwa na hati miliki ya ardhi waliyopewa mwaka 1941 na kuisha 1974 (miaka 33). Hakukuwa tena na marejesho kwa kabidhi wasii mkuu tangu 1965 hadi mwaka 2012, miaka 47 baaye ndipo walipojitokeza na kujaza 'returns' za tangu 1970 hadi 2007 wakidai ndio wadhamini. Tarehe 5/1/2012 kumbukumbu zinaonyesha kuwepo na kikao cha bodi ya wadhamini kuhamisha udhamini kwenda kwa wadhamini hawa wapya ' Returns' zote hizo zikiwasilishwa kwa kabidhi wasii siku moja , tarehe 22/11/2012!

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza mambo yafuatayo yafanyike:-

1) Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi azuie haraka iwezekanavyo mchakato huu haramu kama bado hati haijatolewa!! Na kama hati mpya imeshatolewa tunamtaka Rais atumie mamlaka yake kubatilisha hati husika!
2) Rais Jakaya Mrisho Kikwete amwajibishe mara moja kiongozi huyu kwa kutumia madaraka yake vibaya na kujiingiza kwenye biashara chafu!
3) Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imchunguze kiongozi huyu sambamba na watendaji wote wa serikali waliotumia vibaya madaraka yao kupotosha ukweli juu ya uhalali wa Mawenzi Sports Club kupewa hati ya kumiliki kiwanja hicho!!

## 4. WIMBI LA UNYAKUZI WA ARDHI TANZANIA: UWEKEZAJI WA DANGOTE NA UKIUKWAJI WA SHERIA YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** Suala la unyakuzi wa ardhi Barani Afrika, na hususan Tanzania, ni suala ambalo limekuwa likizungumzwa na Kambi ya Upinzani kwa kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wa bunge hili. Na msingi wa hoja ya kuitaka Serikali kulinda ardhi yetu dhidi ya unyakuzi huo, unatokana na uhalisia kwamba; idadi ya watanzania inaongezeka na ardhi yenye rutuba inazidi kupungua. Aidha, mahitaji ya chakula yanaongezeka kwa kasi duniani. Kwa mujibu wa Taarifa Makisio ya Idadi ya Watu Duniani ya mwaka 2012, inatarajiwa kwamba iifikapo

mwaka 2050, mahitaji ya chakula duniani yataongezeka kwa 70% kutokana na ongezeko la idadi ya watu diniani kutoka bilioni 7.2 mpaka bil 9.6[13]

**Mheshimiwa Spika,** Kudhihirisha umuhimu wa jambo hili, taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Chama Wabunge wa nchi wananchama wa Jumuiya ya Madola (CPA); katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai 2014 hadi 16 Januari 2015 (UK 21) ilieleza namna suala la unyakuzi wa ardhi linavyojadiliwa kwa kina katika vikao vya Kamati na Bunge la Afrika na kwamba Bunge la Afrika limesisitizia kwamba Umoja wa Afrika uweke mikakati bora katika kushughulikia suala la ardhi barani Afrika kwa manufaa ya waafrika na nchi moja moja iweke mikakati na kuboresha sheria na taratibu za ugawaji bora wa ardhi kwa wageni.

**Mheshimiwa Spika,** Kuonyesha umakini wetu, kabla hata hoja hii haijaanza kujadiliwa katika ngazi ya CPA, miaka 5 iliyopita kambi ya upinzani tuliitaka serikali hii ya CCM, kufanya ukaguzi wa ardhi( land auditing )nchi nzima, ili kuliwezesha Taifa kujua kila kipande cha ardhi na matumizi yake!! ili tuweze kama Taifa kuweka mipango thabiti ya matumizi bora ya ardhi kwa manufaa ya Taifa na watu wake.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ikiyajadili haya, na wakati Kamati yako teule ya Bunge iliyopewa jukumu ya kufanya utafiti juu ya kasi ya migogoro baina ya wakulima na wafugaji, wananchi na wawekezaji na wananchi na hifadhi za Taifa wakiainisha uhaba wa ardhi na mipango mibovu ya matumizi ya ardhi kuwa ndio chanzo cha migogoro husika, hivi karibuni tumeshuhudia bilionea namba moja

[13] World population Prospects:The 2012 Revision

Afrika, Alhaji Aliko Dangote akikabidhiwa hekta 2,500 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ili ajenge bandari itakayotumika kusafirisha saruji kutoka katika 'kiwanda chake' cha Saruji kwenda ndani na nje ya nchi .

**Mheshimiwa Spika,** Bilionea huyu amekabidhiwa eneo la ufukwe wa bahari ya hindi, katika kijiji cha Mgao, Kata ya Maumbu, Tarafa ya Mayanga, Wilaya ya Mtwara vijijini, ambapo atajenga 'bandari yake' ya kisasa kwa ajili ya kusafirisha ' saruji yake' itakayozalishwa kwenye kiwanda chake kikubwa kinachojengwa katika kijiji cha Msijute.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa taarifa ambazo zilizagaa kwenye vyombo vya habari (ambazo hazijakanushwa na chombo chochote cha serikali, akiwamo waziri mwenye dhamana katika masuala ya ardhi), Mwenyekiti wa Kijiji cha Mgao, ndugu Abrahaman Shaa ndiye aliyemkabidhi mfanyabiashara huyo ardhi. Mheshimiwa Spika, taarifa zinazidi kueleza kwamba ardhi hiyo - hekta 2500 (sawa na ekari 6,600/-) ilitolewa bure kwa mfanyabiashara huyo, kwa ahadi kwamba wanakijiji hao watajengewa shule na hospitali!

**Mheshimiwa Spika,** Ni aibu kwa Serikali kutoa ardhi yenye thamani kubwa…iliyopo ufukweni (prime area) bure kwa kubadilishana na 'ujenzi wa shule na hospitali. Hii haina tofauti na kubadilishana dhahabu na kipande cha kanga!! au haitofautiani na wale waliopokea vipande vichache vya kaniki wakawauza mababu zetu utumwani. Kweli karne hii ya 21 Serikali inafanya ***barter trade****???!!!* Ina maana sasa Serikali imeshindwa kutoa huduma za jamii kwa wananchi wake hivyo inagawa ardhi yetu ili iwezeshwe na wageni kutoa huduma hizo? Kuna tofauti gani na kusema Serikali imewekwa mifukoni mwa wawekezaji?? Hii ni aibu na ni fedheha ya mwaka kwa Serikali.

## 5. UKIUKWAJI WA SHERIA YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Ardhi ya Kijiji ya mwaka 1999 inatoa mamlaka kwa Halmashauri ya kijiji kusimamia ardhi yote ya Kijiji. Halmashauri ya Kijiji si mmiliki wa ardhi ya kijiji bali ni mdhamini aliyepewa wajibu wa kusimamia ardhi yote ya kijiji. Sheria ya Ardhi imetoa ukomo wa mamlaka ya Halmashauri ya kijiji kugawa ardhi. Na itagawa ardhi husika baada ya kuruhusiwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji ambao una mamlaka ya kupokea, kujadili na kuyafanyia maamuzi masuala kuhusu ugawaji wa ardhi. Hata huo Mkutano Mkuu wa Kijiji, una ukomo wa mamlaka wa kugawa ardhi. Baada ya kupokea maombi ya ardhi, kwa mujibu wa Sheria No.5 ya mwaka 1999, ina uwezo wa kugawa kati ya ekari 100-500 tu swa na (hekta 38- 190)tu!

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili yafuatayo:

i. Utaratibu uliotumika kumpatia Dangote ardhi ya uwekezaji ulikuwa ni wa kisheria au la?
ii. Je, kulikuwa na mahitaji halisi kutoa ya ekari 6,600 ya ardhi ya wananchi kama hoja ilikuwa ni kujenga bandari binafsi ya kumwezesha kusafirisha simenti toka kwenye kiwanda chake kwenda ndani na nje ya nchi? Msingi wa swali hili unatokana na ukweli kwamba eneo la ardhi lililochukuliwa ni kubwa mno ukilinganisha na mahitaji halisi ya eneo la ujenzi wa bandari.

## 6. MIGOGORO YA ARDHI: ISHARA YA KUSHINDWA KWA CHAMA CHA MAPINDUZI

**Mheshimiwa Spika,** kushindwa kwa Chama cha Mapinduzi

kunatokana na ukweli kwamba migogoro baina ya wakulima , wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi imedumu kwa muda mrefu licha ya kwamba nchi yetu ina sera, mikakati na sheria kwa ajili ya kusimamia masuala ya ardhi .Uzembe huu ulibainishwa pia na taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza sababu za migogoro ya ardhi nchini ( Taarifa ilitolewa 6/2/2015). Kamati hii ilibainisha kwamba katika mapitio ya nyaraka mbali mbali waligundua kwamba kuna migogoro ambayo ilianza toka mwaka 1966 (kijiji cha Mabwegere na majirani), haijapatiwa ufumbuzi mpaka sasa [14](Miaka 49 iliyopita).

**Mheshimiwa Spika,** usugu huu wa serikali ya CCM uliendelea kuthibitika kufuatia maelekezo yaliyotolewa na aliyekuwa waziri Mkuu na Makamu ya kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , Ndugu, Joseph Sinde Warioba kwa barua ya tarehe 19/2/1986 iliyokuwa inamwelekeza Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Vijijini kushughulikia matatizo ya wakulima na wafugaji katika kijiji cha Kambala. Licha ya kupewa siku saba (7) kuanzia tarehe 22.2.1986 hadi 1.3.1986 za kutatua mgogoro husika, mpaka sasa (miaka 29) migogoro kati ya wakulima na wafugaji wa kijiji cha Kambala umeendelea kukua na kusababisha vifo, uharibifu wa mali ,uvunjifu wa amani na kuathiri uzalishaji mali.

**Mheshimiwa Spika,** kushindwa kwa CCM kunaendelea kudhihirishwa na mateso wanayokumbana nayo wananchi wa mkoa wa Tanga,ambao kwa kipindi kirefu sana wamekuwa waadilifu na wateja wazuri wa CCM kwa kukipa 'ushindi' unaoitwa wa kishindo katika chaguzi mbali mbali! Mnamo tarehe 1/5/1985 katika sherehe ya wafanyakazi ya Mei Mosi iliyofanyika Tanga, Baba wa Taifa mwalimu Julius K. Nyerere alitoa agizo

---

[14] Barua yenye kumbukumbu namba P. 1/13/244 , kutoka kwa Mkuu wa wilaya (area Commissioner ) ya Kilosa wa wakati huo kwenda kwa viongozi wa wamasai kuhusu ugomvi wa wafugaji wa kimasai unaohusisha kijiji cha Mabwegere na vijiji jirani

kwa mashamba ambayo yameshindwa kuendelezwa na hivyo kugeuka msitu wapewe wananchi wasio na ardhi ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia kauli ya baba wa Taifa, iliundwa kamati ndogo iliyowajumuisha Ndugu. Ibrahim J. Shemdoe, Ndugu Omari S.O Mduruma na Ndugu S. Saidi ilioyopewa jukumu la kuzungukia mashamba yote yaliyotelekezwa na kutoa mapendekezo ya kiasi gani cha ardhi kitwaliwe kwa matumizi ya umma. Baada ya uchunguzi wake wa kina ilipendekezwa vijiji vyenye uhaba mkubwa wa ardhi vimegewe jumla ya **hekta 15,612** kutoka mashamba ya Mamlaka ya Mkonge Tanzania (MTT).Wilaya ambazo zilikuwa zinufaike na mchakato huu ni Muheza , Korogwe , Lushoto, na Pangani!

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyo ada ya Serikali ya CCM, toka mwaka 1985, mpaka sasa mchakato huu haujafanyika kwa ufanisi. Mpaka sasa hivi kuna Mgogoro mkubwa sana unaofukuta katika wilaya ya Muheza! na waahanga wakuu ni wanavijiji wa Mgome, Mpapayu, Kigongomawe na Kwamnyefu. Mgogoro huu ni kati ya ndugu **Khamisi Kindoroko** 'mwekezaji' anayemiliki shamba la **KUMBURU Estate** ambalo liko chini ya **Silver General Distribuitors Ltd** na wananchi!

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati ya wananchi iliyoundwa kipindi hicho shamba la Kumburu lenye ukubwa wa **hekta 2,904** lilitakiwa limegwe **hekta 904** …mchakato ambao haujafanyika mpaka sasa!

**Mheshimiwa Spika,** licha ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Mhe. Ole Medeye kufanya ziara ya kikazi katika wilaya ya Muheza kwa lengo la kushughulikia maswala mbali mbali ya ardhi likiwemo shamba la Kumburu na kutoa maelekezo ya utatuzi kwa Mkuu wa wilaya kwa barua yenye kumbukumbu namba LD/1464 Vol. III ya tarehe

15/05/2012 kwa lengo la kuumaliza mgogoro husika, kama ilivyotokea kwa Mkuu wa wilaya katika tukio la mgogoro wa ardhi mwaka 1966 na 1986 chini ya CCM ndivyo ilivyotokea mwaka mwaka 2012! Kikubwa alichokifanya mwakilishi wa Rais, badala ya kutatua mgogoro alikwenda kuwaita wananchi MBWA!

**Mheshimiwa Spika,** ninapowasilisha hoja hii baadhi ya wanakijiji waliokuwa mstari wa mbele kupigania haki yao wamebambikiziwa kesi za mauaji ! wengine mpaka sasa wapo Geraza la Maweni! kama ilivyo kwa maelefu ya watanzania wengine wanaosota kwenye magereza kwa kesi za kubambikiwa na utawala wa CCM, bila kusikilizwa. Inasemekana jalada (P.I No. 4/2014) liko kwa mwanasheria mkuu wa serikali .

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya upinzani inamtaka Waziri wa ardhi alieleze Bunge hili tukufu, ni lini anatarajia kuimaliza migogoro hii sugu!!!

Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imetoa uamuzi gani kwa kufuatia adha kubwa na mateso wanayokumbana nayo wananchi wa **Tarafa ya Olboloti Kibaya, Kiteto,** ambapo wananchi wanalalamikia kamata kamata inayofanywa na Askari Polisi, inayokwenda sambamba na kuwachapa viboko na kuwalazimisha kutafuna mbegu za mahindi na alizeti na kuzimeza!!

**Mheshimiwa Spika,** wananchi wanapata adhabu hii kwa sababu tu ya kufanya shughuli za kilimo!!Shughuli ambazo wamekuwa wakizifanya toka mwaka 1998! Kambi ya upinzani inatambua kwamba iliundwa Tume ya maridhiano chini ya Ofisi ya waziri kuu kwa madhumuni ya kulitafutia ufumbuzi suala hili!!Na kwamba Tume husika imeshatoa taarifa kwa Waziri Mkuu! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu.

## 7. MGOGORO WA ARDHI KATI YA CDA NA WANACHI – MANISPAA YA DODOMA

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu sasa kati ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) ambapo wananchi siku zote wamekuwa ndio wahanga wakubwa na hakuna wa kuwasaidia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba mnamo tarehe 30 Machi, 2015 CDA ilitoa notisi ya kuvunjwa kwa nyumba tano za wananchi ili kupisha ujenzi wa kituo cha afya.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya notisi hiyo, wananchi waliandika barua ya malalamiko kwa CDA ya kutaka kulipwa fidia kwa nyumba zao na maendeleo mengine waliyokuwa wameyafanya katika maeneo yao. Jambo la kushangaza ni kwamba wakati wananchi hao wanasubiri majibu ya barua zao, CDA iliendesha operesheni ya kubomoa nyumba zao mnamo tarehe 6 Mei, 2015 bila taarifa yoyote. Hadi muda huu ninaposoma hotuba hii, wananchi hao wanaishi chini ya miti na hawajui haki yao itapatikana wapi. Mpaka tarhe 1 Juni, 2015, Notisi nyingine za ubomoaji zimeendelea kutolewa na CDA kwa sababu za kupisha ujenzi wa huduma za jamii kama vile shule, hospitiali na Barabara.

**Mheshimiwa Spika,** dhoruba hii ya kuvunjiwa nyumba bila fidia inayofanywa na CDA ilikuwakuba pia wakazi wa Eneo la Msangalalee ambapo, mwaka 2014 CDA ilitoa notisi ya kuvunja nyumba 35 katika eneo hilo bila fidia ili kupisha ujenzi wa barabara. Wananchi walifungua kesi mahakama kuu kanda ya Dodoma kupinga agizo hilo la CDA. Mahakama ikasikiliza na kutoa zuio kwa CDA kuvunja nyumba hizo hadi kesi ya msingi itakapomalizika. Chaajabu ni kwamba CDA ilivunja nyumba hizo bila kujali amri ya mahakama. Kuvunjwa kwa nyumba hizo kuwaliwaacha wananchi takriban 170 bila makazi.

**Mheshimiwa Spika,** Dhoruba hiyo iliendelea kuwakumba wananchi wa Eneo la Msalato ambapo zaidi ya wananchi 1000 walichukuliwa mashamba na nyumba zao na Serikali kwaajili ya kupisha ujenzi wa uwanja wa ndege. Tathimini ilifanyika tangu 2011, wananchi wamezuiwa kulima na/au kuendeleza maeneo yao kwa miaka yote bila kupata fidia wanayostahili kisheria. Watoto wameshindwa kwenda shule kwasababu ya kuvurugwa kwa mfumo wa uchumi wa familia hizi. Kuna watu ambao wamepoteza maisha kwa kukosa kipato kutokana na serikali kushikilia Ardhi yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu fidia kwa Wakazi wa Msalato ambao wanapisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege, aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Harison Mwakyembe alishawaahidi wananchi hao kupitia barua yake kumb. Na. DE 20/230/01 ya tarehe 9 Mei, 2013 kwamba watalipwa fidia zao katika mwaka wa fedha 2014/15. Kwa mujibu wa barua hiyo, Mhe, Mwakyembe alisema Mthamini Mkuu wa Seriklai ameshakamilisha zoezi la thathmini na kwamba kiasi cha takriban shilingi bilioni 3 zinahitajika kuwalipa wananchi 980 katika eneo la Msalato.

**Mheshimiwa Spika,** Mpaka sasa sasa mwaka wa fedha 2014/15 unamalizi fidia hiyo haijalipwa kama Mhe. Mwakyembe alivyoahi. Kutokana na wananchi hao kumlalamikia Waziri Mkuu, juu ya ucheleweshwaji wa fidia hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu ilimwandikia Waziri wa Uchukuzi barua yenye Kumb. Na. PM/P//2/569/79 ya tarehe 21 Januari, 2015 ikiitaka Wizara ya Uchukuzi ilifanyie kazi zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi hao na kumpa taarifa Mhe. Waziri Mkuu juu ya utekelezaji wa zoezi hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri

wa Ardhi alieleze Bunge hili amechukua hatua gani kuhakikisha kwamba Wizara ya Uchukuzi inalipa fidia hiyo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri wa Ardhi alieleze Bunge hili kuhusu mambo yafuatayo:

i. Ni sera ya Serikali hii ya CCM kuwabomolea wananchi nyumba zao bila kuwalipa fidia?
ii. CDA ilivyowapa wananchi viwanja haikuwa na Master Plan kujua ni sehemu gani patajengwa shule, hospitali au barabara kiasi cha kuja kuwasababishia wananchi hasara na umasikini wa kudumu kiasi hiki?
iii. CDA inatoa wapi kiburi cha kuwabomolea wananchi nyumba zao hovyohovyo bila hata kutii amri ya Mahakama?
iv. Serikali inatoa kauli gani juu ya wananchi waliobomolewa nyumba zao na CDA ambao mpaka sasa wanaishi chini ya miti?
v. Ni lini Serikali itatoa fidia kwa wananchi waliovunjiwa nyumba zao katika Manispaa ya Dodoma kwa ajili ya kupisha miradi ya maendeleo?

## 8. MGOGORO WA ARDHI KATIKA KIJIJI CHA KIFANYA HALMASHAURI YA MJI WA NJOMBE.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo kwa Mgogoro wa Ardhi katika kijiji cha Kifanya ndani ya Halmashauri ya Mji wa Njombe, ulionzishwa na kauli ya Mkuu wa Wilaya Bi. Sara Dumba tarehe 13/06/2014 wakati akifanya uzinduzi wa vitalu vya chai - Mawolo, Kijiji cha Kifanya. Kauli ya Mkuu wa Wilaya ilikuwa ni kwamba wananchi walime chai na Halmashauri za vijiji zigawe maeneo kwa wakulima wadogo. Kauli hii ilipelekea halmashauri

ya kijiji kuvunja sheria ya ardhi na kanuni zake kwa kugawa ardhi pasipo kuzingatia sheria.

**Mheshimiwa Spika,** ardhi iligawiwa pasipo kuwepo Mkutano Mkuu wa kijiji na kuhusisha wananchi kufanya maamuzi. Mkutano wa ugawaji ardhi ambao ulifanyika tar 15/06/2014 ambao ulihudhuriwa na wananchi 15 tu haukuonesha mahudhurio ya jamii ya wafugaji hata mmoja pamoja na kuwa na wajumbe wachache kutoka katika jamii ya wakulima.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tar 31/11/2014 Halmashauri ya Kijiji iligawa Ardhi Jumla ya hekta 221. Baada ya eneo hilo kugawiwa kwa wananchi na wawekezaji kwa barua za Mwenyekiti wa Kijiji na nakala kupelekwa kwa Mkuu wa Wilaya ikisema…. ***''nimetekeleza agizo lako la kugawa mashamba ya chai''*** baada ya kufanyika zoei la ugawaji wa ardhi na shughuli za kilimo kuanza, yalijitokeza malalamiko ya wafugaji kudai maeneo yao yaligawiwa pasipo kuwahusisha wao kama wafugaji. Malalamiko hayo yalitolewa katika kikao cha wafugaji mnamo tar 28/02/2015 na kudai kuvunjiwa eneo lao la Igaba, Kuvunjiwa zizi la chanjo bila taarifa ambapo eneo hilo liligawiwa kwa wakulima, Kutishiwa amani na wakulima waliogawiwa eneo la wafugaji.

**Mheshimiwa Spika**, Mkuu wa wilaya ambae alitoa agizo la utoaji ardhi ameshindwa kutatua mgogoro huu hadi sasa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Mkuu wa Wilaya anahusika pia kujipatia eneo kwa majina ya tofauti ili kuweza kujinufaisha yeye binafsi. Mkurugenzi wa Halmshauri ya Mji pia ameshindwa kutatua mgogoro huu kwa kuwa anamlinda Mkuu wa Wilaya. Matokeo yake, kuna uhasama mkubwa baina ya Wakulima na Wafugaji jambo ambalo limesababisha kutoweka kwa amani na utulivu kwa makundi haya ya jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu hapa ili wananchi wa Njombe, Kijiji cha Kifanya chenye wakulima na wafugaji kujua nini hatma ya ardhi yao. Pili ni hatua gani stahiki zimechukuliwa baada ya malalamiko ya wananchi kupelekwa kwa Mkurugenzi chini ya kamati ya Uchunguzi ya Kijiji ambayo imeonesha uvunjifu wa sheria ya ardhi uliofanywa na mwenyekiti wa Kijiji Kifanya pamoja na Mkuu wa Wilaya?

## 9. MIGOGORO YA ARDHI BAINA YA WANANCHI NA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

**Mheshimiwa Spika,** Suala la migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Wizara ya Maliasili na Utalii sio jipya katika Bunge lako tukufu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelizungumzia mara kadhaa kama sauti ya wasio na sauti, na kamwe, Kambi ya Upinzani haitachoka kulizungumzia kutokana na vipigo mauaji, na uharibifu wa mali unaoendelea kuwakumba wananchi, huku Wizara ya Maliasili na utalii ikiratibu na kusimamia uhalifu huo dhidi ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kumbu kumbu zinaonyesha kwamba toka mwaka 1994 wananchi hawa wanahangaika bila mafanikio! Hakuna ofisi ya serikali hii ya CCM yenye mamlaka ya kushughulikia suala hili ambayo hawajafika!! Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inajua (suala hili lilishughulikiwa na Ndugu George M. Masaju, (Mwanasheria Mkuu wa sasa, kipindi hicho akiwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali), Wizara ya Ardhi inajua, wananchi hawa walishafika mpaka hata ofisi ya Rais!! Mheshimiwa Spika, wewe ni shuhuda wa malalamiko ya wabunge dhidi ya ukatili unaofanywa na wanaojiita maafisa wanyamapori na wahifadhi wa misitu!!

**Mheshimiwa Spika,**mawasiliano baina ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya tarehe 21/4/1994 yenye kumbukumbu namba MD/F.40/1/28 juu ya malalamiko ya kitongoji cha Nzansa, kijiji cha Chanika, wilaya ya Ilala kufukuzwa kwenye eneo linalopakana na hifadhi ya msitu wilaya ya Kisarawe, yanakiri kwamba wanakijiji walihamia hapo tangu mwaka 1954, wakati eneo la misitu lilikuja kupimwa mwaka 1993 na kwa kusimamiwa na Afisa Maliasili wa Mkoa wa Pwani, Ndugu Kessy.

**Mheshimiwa Spika,** barua toka ofisi ya Rais, ya tarehe 10/6/2008 yenye kumbukumbu namba CEA 110/302/IV/01 kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi juu ya malalamiko ya wakulima wa (Chanika-Nzasa), pamoja na mambo mengine, inakiri kwamba Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi ilianzishwa na Gavana E.F Twining kwa tangazo la serikali Na. 306 lililochapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 septemba 1954. Na kwamba Tangazo hilo liliweka Mipaka ya Hifadhi ya msitu wa Kazimzumbwi kwa kutaja vipimo vya maeneo ya Mipaka (Nakala ya tangazo imeambatanishwa).

**Mheshimiwa Spika** ukipitia ramani (Kama ilivyotolewa na Wizara ya Ardhi-wizara yenye dhamana ya kusimamia upimani na utayarishaji wa ramani nchini),ni ukweli ulio dhahiri kwamba wananchi hawa wako nje kabisa ya mpaka wa hifadhi!! Katika mbinu za kitapeli na uharamia dhidi ya wananchi wizara ya maliasili na utalii imekuwa ikitumia Government Notice No. 156/1997 iliyochapishwa katika Gazeti la serikali la tarehe 20 Mei 1997 (The Kazimzumbwi Forest Reserve (Removal of Unlawful Occupants and cessation of unlawful Activities ) Rules 1997 wakidai wananchi hao wamevamia msitu!!

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa amri hii(kwa tafsiri) unawahusu tu wale wananchi walio ndani ya hifadhi! Wizara ya maliasili na utalii inatumia ubabe wa amri hii, pasipo kuwa na ujasiri wowote wa kufanya rejea ya Tangazo lililoweka mipaka ya hifadhi!. Cha kushangaza zaidi vijiji vya Vibura (Nzasa), Maguruwe na Vijibweni ambavyo viko ndani ya hifadhi havijaguswa!!

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ambazo Kambi ya Upinzani inazo ni kwamba, kuna mchezo mchafu uko nyuma ya pazia. Nasema hivi kwa sababu wakati Wizara hii hii inafukuza na kuua wananchi kwa barua yake yenye kumb. Na. MTNREF/F/40/5/67 ya tarehe 30 Desemba 199, ilimjulisha Mwenyekiti wa Chama Cha Msaada wa Kisheria, Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwamba wananchi wa Nzansa wako nje ya Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi na hivyo wananchi hao wasihofu kwa kuwa hawahusiki na zoezi la kuwaondoa wavamizi wa msitu!

**Mheshimiwa Spika,** Nikinukuu barua tajwa hapo juu, yenye kichwa cha habari ***"Kazimzumbwi Forest Reserve Apprehension of Nzasa Villagers"***, kifungu cha pili kinasema, hivi: nanukuu,

" *It is true that the Government intends to evict encroachers from Kazimzumbwi Forest Reserve and wish to assure you that Nzasa Village is outside the Reserve, as such Nzasa Villagers have nothing to fear about the intended evictions*" mwisho wa kunukuu.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kujiuliza: kama Nzasa Chanika ipo ndani ya

eneo la hifadhi ya masitu (ambayo iko kisarawe, mkoa wa Pwani):

i) Mbona ni kijiji kinachotambulika rasmi na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (jimbo la Ukonga)?

ii) Kama eneo la Kijiji cha Nzasa kimo katika hifadhi ya msitu mbona Kamishna wa madini amekuwa akitoa vibali vya machimbo ya mchanga katika eneo hilo?

iii) Ikiwa eneo la kijiji cha Nzasa limo katika hifadhi ya misitu inakuwaje basi maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya huduma ya jamii katika kijiji hicho sasa hivi yanachukuliwa na watu wengine kwa ajili ya shuguhuli nyingine hatua ambayo imelalamikiwa na wakulima wa kijiji hicho cha Nzasa?

iv) Na ikiwa kijiji cha Nzasa kimo katika eneo la hifadhi ya msitu, mbona wananchi wakulima wakazi wenyewe wa kijiji hicho ndio wako mstari wa mbele kutaka hatua zichukuliwe ili kuzuia uharibifu wa mazingira?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo kimsingi ndiyo yenye mamlaka ya usimamizi wa ardhi wa nchi hii kuliangalia suala hili kwa jicho la ziada. Wizara ya ardhi ina nyaraka zote zinazohusiana na mgogoro huu. Kama waziri kivuli niliwasilisha nyaraka nyingine kwa msisitizo!!Kuna upotoshwaji mkubwa sana unafanywa na wizara ya Maliasili na Utalii, na mbaya zaidi hata kamati yako ya Bunge ya ardhi na maliasili inapotoshwa na Wizara!.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga (ambaye naye alipambana sana bila mafanikio), Marehemu Eugine Mwaiposa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mhe. Waziri atoe kauli ya serikali hapa Bungeni juu ya mustakabali wa wananchi hawa.

**Mheshimiwa Spika,** nyaraka za migogoro ya Msitu wa Kazimzumbwi kati ya wananchi ha Wizara ya Maliasili na Utalii zimeambatanishwa katika hotuba hii katika ***vielelezo na. 4,5,6,7 8,9,10 na 11.***

## 10. JESHI NA UPORAJI WA ARDHI KIJIJI CHA TONDOLONI (MKOA WA PWANI) NA KIJIJI CHA IHUMWA (DODOMA)

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kazi nzuri inayofanywa na jeshi letu la kulinda mipaka ya nchi yetu. Halikadhalika, kazi nzuri inayofanywa katika kushiriki katika operation mbali mbali za kulinda Amani katikabara la Afrika na kwingineko duniani. Hata hivyo, Bunge lako tukufu limeshuhudia malalamiko ya wabunge kwa upande ( kama wawakilishi wa wananchi kwa upande mmoja ) na serikali (kupitia wizara ya ulinzi kwa upande mwingine), wabunge wakidai jeshi liinangia kwenye maeneo ya raia, serikali kwa upande mwingine ikidai wananchi ndio wanaovamia maeneo ya jeshi. Hoja zote mbili zina ukweli kwa namna Fulani.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepokea taarifa ya migogoro mbali mbali inayolihusu jeshi kuvamia maeneo ya wananchi, kutokana na ufinyu wa muda tutaongelea migogoro '2'

(Kijiji cha Tondoloni- Kisarawe Mkoa wa Pwani na Kijiji cha Ihumwa, Mkoa wa Dodoma) ambayo inafukuta sana . Ni matarajio yetu, serikali kupitia wizara ya ardhi na wizara ya ulinzi, itatumia busara ya hali ya juu kumaliza fukuto hili!! Hatuwezi ruhusu walinzi wetu wa Amani ambao tunawategemea wawe chanzo cha uvunjifu wa amani nchini!.

**Mheshimiwa spika,** Kijiji hiki cha Tondoloni, kilianza mwaka 1960, wananchi walianza kuishi hapo kabla ya uhuru. Mwaka 1986 wanajeshi walikwenda kuomba kufanya tathmini ili kuwalipa fidia kwa madhumuni ya kuongeza eneo la jeshi. Tathmini ilifanywa ikiwahusisha **wanakijiji 1, 508.** Hakuna fidia yoyote waliyolipwa, baada ya malalamiko Wananchi walipokea barua toka ofisi ya ardhi na makazi ambayo ilielekeza wananchi walipwe ndani ya miezi mitatu na kwamba miezi mitatu ikipita haitambuliki tena. Tathmini husika ilikuwa tarehe 21/10/1992.

**Mheshimiwa Spika,** Hakuna fidia yoyote iliyolipwa, mpaka mwaka 1998 ambapo wanajeshi walikwenda kuharibu mazao ya wananchi na kukata miti ya kudumu. Taarifa ilitolewa kwa Mkuu wa mkoa kipindi hicho Prof. Philemon Sarungi. Mchakato wa utatuzi ulikwama baada ya Mkuu huyo wa Mkoa kuhamishwa kituo cha kazi. Mwaka 1999 barua iliyotoka ofisi ya afisa tawala mkoa ilielekeza kwamba endapo serikali ilikuwa inahitaji eneo la wananchi, lazima tathmini ifanyike upya. Kwa maelezo ya wananchi, hakuna tathmini yoyote iliyofanyika; ila kilichoendelea ni wananchi kupigwa, kuharibiwa mali zao na JWTZ kikosi No 83, wananchi wakipeleka malalamiko yao katika mamlaka mbali mbali za serikali …hawasikilizwi!!

**Mheshimiwa Spika,** mpaka sasa kuna mgogoro mkubwa, wananchi wanapigwa risasi (uthibitisho upo), nyumba zinavunjwa, mazao ya kudumu yanang'olewa...wananchi wanaishi katika ardhi yao kama wanyama! (Nyaraka zote zimeambatanishwa kama sehemu ya hotuba hii).

**Mheshimiwa Spika,** kadhia kama hii imekikumba pia kijiji cha Ihumwa, ambapo jeshi la wananchi JWTZ wamechukua mashamba ya wanakijiji na kuanza kujenga nyumba pasipo kuwalipa fidia. Kijiji hiki kilisajiliwa kwa sheria za ardhi na vijiji mwaka 1971, kikiwa na hati miliki Na. DO/KJ/IHM/353. Ikumbukwe kwamba Wananchi wa maeneo haya wanategemea kilimo kwa maisha yao hivyo kuchukua ardhi yao bila fidia ni kutaka kukatisha maisha yao.

**Mheshimiwa Spika,** kuthibitisha kwamba eneo husika halikuwa la jeshi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina barua toka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ya tarehe 30/1/1987 na tarehe 1/1/1989, kwenda kwa mwenyekiti wa kijiji cha Ihumwa . Barua husika inaomba eneo la kijiji cha ihumwa (kwa matumizi ya Muda) kwa ajili ya mafunzo ya askari waenda kwa miguu daraja la tatu katika eneo la kijiji kaskazini mwa barabara kuu iendayo Dar es salaam .(Barua husika zimeambatanishwa). Wanakijiji hawa wamehangaika bila mafanikio na hata walipowasilisha taarifa wizara ya ardhi, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa, wanashangaa walipoiandikia barua wizara kuikumbusha juu ya mgogoro husika, walijibiwa kwamba waliitwa kutoa ushahidi lakini hawakutokea (jambo ambalo sio kweli)!

**Mheshimiwa Spika,** Kitu ambacho kinashangaza zaidi, ni kwamba; barua ya Wizara ya ardhi, ya tarehe 27 Novemba 2014 yenye kumbukumbu namba MLHHSD-C/PODM/76, inaeleza kwamba jeshi la wananchi liliwasilisha Ramani iliyoidhinishwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani tarehe 30/05/1985. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji: Kama ramani ilishabadilishwa (kienyeji mwaka 1985 bila kukishirikisha kijiji) iweje basi jeshi hilo hilo, mwaka 1987 kupitia kwa Captain ALLY PSC ( KNY Kamanda Rejimenti) na na mwaka 1989 kupitia Captain R.J. P.S.C waandike barua ya maombi ya ruhusa ya kufanya mafunzo? Utaombaje ruhusa kwenye eneo ambalo tayari ni la kwako?

**Mheshimiwa Spika,** kama kweli eneo husika lilishatwaliwa na jeshi toka mwaka 1985, (kama maelezo ya wizara ya ardhi yanavyoainisha, iweje basi mwezi Februari mwaka 2013, Brigedia Mndeme amteue Captain Manyiga na Coplo Halid na CP Kibonde kufanya uhakiki wa mashamba wakishirikiana na viongozi wa kijiji na wakulima kwa madhumuni ya kulipa fidia? Kambi Rasmi ya Upinzani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa migogoro ya ardhi kati ya jeshi na wananchi wa Tondoloni mkaoni Pwani na Ihumwa mkoani Dodoma, tazama ***vielelezo na. 11, 12,13 na 14***

## 11. UVAMIZI WA ARDHI YA TAZARA

**Mheshimiwa spika,** wakati tukishuhudia wizi , udanganyifu na ufisadi

katika zoezi la kuuza nyumba za TAZARA (Tanzania Zambia Railway Authority) kama ilivyobainishwa katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, katika Wizara ya Uchukuzi, Mhe. Mosses Machali, mali za serikali kugeuzwa shamba la bibi imeikumba pia ardhi ya Tazara ambayo imegawanywa vipande vipande .

**Mheshimiwa Spika,** Ardhi hii iliachwa wazi kwa ajili ya matumizi ya baadaye pale ambapo mamlaka ingepanuka kibiashara hivyo kuweka vitegauchumi vingine zaidi, halikadhalika kwa matumizi ya umma ( masoko,parking ,viwanja vya michezo na bustani).

**Mheshimiwa Spika,** ni jambo la kawaida kwa serikali ya chama cha mapinduzi kushindwa kulinda mali ya umma.Uchunguzi uliofanywa katika eneo la Dar es salaam (Yombo – Kurasini) umegundua kwamba kuna nyumba zaidi ya 600 zimejengwa ndani ya ardhi ya mamlaka. Mgololo zaidi ya hektab 40 za ardhi imevamiwa na sasa limepandwa miti na kuna makazi ya watu pia. Uvamizi wa aina hii umeshamiri pia Makambako, Ifakara na maeneo mbali mbali ambayo yaliachwa mahsusi kwa malengo fulani. (Taarifa ya uchambuzi husika imeambatanishwa kama sehemu ya hotuba hii). Mheshimiwa Spika katika kudhihirisha kwamba wavamizi walikuwa wanajua wanachokifanya mawe yaliyokuwa yanaainisha mipaka (beacons) yameng’olewa ili kufuta ushahidi.

**Mheshimiwa spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka waziri wa ardhi kuliambia Bunge hili tukufu, katika miezi 3 iliyobaki ya utawala wa

CCM, atalishughulikiaje tatizo hili ili kuokoa ardhi hii muhumu.

## 12. WAMILIKI WA MASHAMBA MAKUBWA HAWALIPI KODI YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** wakati migogoro ya ardhi ikifukuta nchi nzima kutokana uhaba wa ardhi kwa matumizi ya shughuli za kilimo na ufugaji, imebainika wamiliki wengi wa mashamba makubwa, wamekuwa wakiikosesha serikali mapato,kwa kutolipa kodi ya ardhi kama matakwa ya Sheria ya Ardhi No.4 ya mwaka 1999 inavyoelekeza.

_**Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa** utafiti uliofanywa na Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam[15] mwaka 2013 kwa kutembelea mashamba 964 yenye ukubwa wa takriban **ekari 3,706,757** umebainisha kwamba wamiliki wa mashamba 642 kati ya mashamba 964 yaliyotembelewa walishindwa kuthibitisha kama wamelipa kodi ama la katika kipindi cha mwaka 2012

**Mheshimiwa Spika,** katika hali inayoonyesha ukosefu wa umakini kwa upande wa serikali, na hususan Wizara ya Ardhi utafiti umebainisha kwamba hakuna uwazi katika malipo ya kodi ya ardhi kutoka kwa wamiliki wa mashamba na kwamba kati ya hao wachache waliosema wamelipa kodi (wamiliki ma mashamba 322) zaidi ya 79% waliishindwa kutoa risiti kuthibitisha hilo, walioweza kutoa risiti ni 13% tu!

[15] An assessment and evaluation of ownership of farms above 50acres in Tanzania Mainland 2013, prepared by department of economics , University of Dar es salaam,2013, Tel 255222410252 Ext.2262, Email doe@udsm.ac.tz

**Mheshimiwa Spika,** halikadhalika utafiti umegundua kwamba 43.47% ya wenye mashamba waliohojiwa walikiri kwamba hawajawahi kulipa kodi ya ardhi toka walipomilikishwa mashamba hayo!. Hii inaonyesha kwamba, hata wale watu ambao wanamiliki ardhi kihalali, uhalali wa umiliki wao una mashaka kutokana na kutokidhi takwa muhimu la kumiliki ardhi husika ambalo ni ulipaji wa kodi ya ardhi.

## 13. KODI INAYOPOTEA KUTOKANA NA UKIUKWAJI WA SHERIA YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 33 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, kinatamka kwamba, mwenye hati miliki anatakiwa, pamoja na masharti ya vifungu vingine vya sheria hiyo, kulipa kodi ya mwaka kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Fedha za Umma (Public Finance Act).

**Mheshimiwa Spika,** kwa idadi pekee ya mashamba yaliyotembelewa, Serikali inapoteza zaidi ya shilingi **bilioni 3.7** kwa mwaka kutokana na kutokusanya kodi ya ardhi. Ikumbukwe kwamba wamiliki wa mashamba wanatakiwa kulipa kodi kiasi cha shilingi 1000tu kwa ekari 1 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** utafiti umeonyesha kwamba kwa mwaka 2012 kati ya shilingi **bilioni 3.7** zilizotakiwa kulipwa wenye mashamba walilipa shilingi **milioni 130 tu (3.5%)** ya kodi yote iliyotakiwa ilipwe! Utafiti huo pia unaonesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotoza kiasi kidogo sana cha kodi ya ardhi duniani .

**Mheshimiwa Spika,** Ukiukwaji huu wa sheria ni sababu tosha ya ya

kuwafutia umiliki wenye mashamba ambao hawalipi kodi ya ardhi. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuwafuatilia wamiliki hawa wa mashamba makubwa ambao hawalipi kodi ya ardhi na kuacha kuwakandamiza watu masikini wa Chasimba, Kapunga na Kigamboni. igamboni n.k

## 14. SOKO LA NYUMBA NA UMUHIMU WA NYUMBA KATIKA KUKUZA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya nyumba katika nchi zilizoendelea inachangia kati ya asilimia 50 mpaka 70 ya Pato la Taifa kwa mwaka. Tanzania inakabiliwa na changamoto ya uhaba mkubwa wa nyumba bora ambao unakadiriwa kufikia nyumba 3,000,000. Pengo la mahitaji ya nyumba linakadiriwa kukua kwa takriban nyumba laki 2 (200,000) kwa mwaka. Upungufu wa nyumba ni mkubwa zaidi sehemu za mjini ambako asilimia 37.5 ya watanzania ndiko wanakoishi. Shirika la nyumba la Taifa likiwa chombo cha serikali, lilitarajiwa kukabiliana na changaoto hii, hata hivyo mzigo wa kodi unakuwa kiwazo kikubwa cha ufanisi wa shirika hili, hali inayopelekea shirika kuhudumia watu wenye kipato cha juu na kipato cha kati.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba la Taifa linakabiliwa na Mzigo wa kodi/makato mbalimbali kama ifuatavyo:

i. 10% ya mapato yao ya mwaka - Mfuko mkuu wa hazina kushindwa kupeleka kunapelekea penalty ya 5%
ii. Kodi ya makampuni ya asilimia 30%
iii. Kulipa gawio la shilingi milioni 300,

iv. Riba kwa mkopo wa ujenzi wa asilimia 16%

v. Hakuna ruzuku ya aina yoyote toka Serikali kuu,

vi. Kodi zingine kama vile; Kodi ya ongezeko la thamni-VAT,Kodi ya Ardhi *(Land rent),* Kodi ya Mengo *(Property Tax),* Kodi ya Zuio*(withholding Tax),* Kodi ya halmashauri (*City Service Levy),* na Kodi ya Veta (*Skills and development levy)*.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka jana Bunge lako tukufu lilipitisha kodi ya zuio (withholding tax)ya 10% . Kodi hii ilianzishwa mahsusi kwa lengo la kuzitaka taasisi za umma, mashirika ya umma, wakala za serikali n.k kuchangia 10% ya mapato yao ya mwaka katika mfuko mkuu wa hazina. Kutokana na takwa hili la kisheria, Shirika la nyumba linalazimika kuazima fedha/kukopa fedha kuweza kutimiza takwa hilo la kisheria kwa sababu faida wanayoipata kwa mwaka ni pungufu ya kiasi cha fedha kinachohitajika.

**Jedwali hapo chini linaonyesha hali halisi baada ya kuanzishwa kwa Kodi ya zuio[16]**

***Kiasi kwa Tshs.***

| | Mahesabu yaliyokaguliwa 2012 | Matarajio 2014 |
|---|---|---|
| Mapato ya mwaka (kabla ya kodi au | 51,949,340,000 | 176,875,348,298 |

[16] Presentation to the Parliamentary committee ,Effects of the New Finance Bill on construction Projects, 22nd August 2013, National Housing Corporation.

| | | |
|---|---|---|
| gharama za uendeshaji) | | |
| Faida kabla ya Kodi | 4,406,753,000 | 9,668,972,714 |
| | | |
| 10% kodi kwa pato la mwaka | **5,194,934,000** | **17,687,534,830** |
| | | |
| Faida baada ya malipo ya 10% | **(788,181,000)** | **(8,018,562,116)** |

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2014 kutokana na mauzo ya nyumba shirika la nyumba linatarajia kupata mapato (Gross Revenue) ya **shilingi 176,875,348,298.** Hii inamaanisha ,watawajibika kuilipa serikali, **shilingi bilioni 17** kama **10%** ya mapato yao ya mwaka kwa kupitia mfuko mkuu wa hazina. Kutokana na ukweli kwamba Shirika la nyumba linakopa fedha za ujenzi kwa Riba ya 16% kwa mwaka, malipo haya ya shilingi bilioni 17 kwa serikali yanaipunguzia uwezo wake wa kukopa kwa shilingi **bilioni 110.5**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya kodi ya zuio kwa Shirika la Nyumba kumepunguza uwezo wake wa kujenga nyumba kwa 40% kwa

mwaka. Kwa taarifa tu, kama Bunge lako tukufu lilikuwa halijui kwa malipo ya hizo shilingi bilioni 17, Shirika la nyumba linapoteza uwezo wa kujenga **nyumba 3,071**(kwa gharama ya shilingi 36 milioni kwa kila nyumba) kutokana na vikwazo katika mzunguko wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ingeweza kupata mapato zaidi kama ingeiruhusu NHC kuwekeza kiasi hicho katika ujenzi wa nyumba. Kwa gharama ya shilingi milioni 36 kwa nyumba 3,071, serikali ingekuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi 26 bilioni kutoka kwenye kodi, achilia mbali faida za kijamii zitakazopatikana kutokana na ujenzi wa nyumba hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Ni muhimu ikaeleweka kwamba mzigo huu wa kodi mbali unaathiri kwa kiwango kikubwa ufanisi wa shirika, una athari kubwa kwa mlaji, mtanzania wa kawaida anayetarajiwa kupanga au kununua nyumba za shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kufanya yafuatayo:

1) Kulisaidia shirika la nyumba kuweza kumiliki sehemu kubwa ya ardhi kwa gharama nafuu au kupewa bure,kwa kufanya hivyo itasaidia kupunguza gharama ya nyumba ambazo zinajengwa kwa ajili ya kuziuza kwa wananchi wa kipato cha kawaida
2) Kuondoa/kupunguza kodi ya vifaa vya ujenzi ili kuwawezesha watanzania kujenga /kununua nyumba bora kwa gharama nafuu.

## 15. MASTER PLAN JIJI LA MWANZA NA ARUSHA

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya upinzani inatambua kazi inayofanywa na wizara ya ardhi yenye madhumuni ya kuendeleza jiji la Mwanza na Arusha. Halikadhalika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba wizara ya ardhi imeingia makubaliano na kampuni ya Singapore Cooperation Services ambayo imepewa jukumu la kutoa ushauri wa kitaalam wa uendelezaji wa jiji la mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano ya awali gharama za utengenezaji wa Master Plan ya jiji la Mwanza zilikuwa **$ 4,131,010.00** (Bila ya kujumuisha Kodi) wakati jiji la Arusha makubaliano ya awali yalikuwa **$ 4,541,210.00**(Bila kujumuisha kodi). Katika hali ya kushangaza , katika jiji la Mwanza gharama zikaongezeka mpaka kufikia **$ 4,483,095** halikadhalika jiji la Arusha gharama zimeongezeka kufikia **$ 4.927.415**. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge sababu za ongezeko hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa kifungu cha 4.1 cha makubaliano baina ya wizara ya ardhi na Mtaalam Mshauri kuhusiana na suala la Kodi (Clarification on tax liabilities issues) ilikubalika kwamba litakuwa jukumu la mtaalam mshauri (Consultant) 'kulipa kodi' na tozo kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi!

**Mheshimiwa Spika,** Katika hali ya kushangaza 'Invoice' (Invoice No: 20114088 ) ya tarehe 18/2/2015 toka kwa Mshauri Mtaalam

(Consultant) kwenda wizara ya ardhi, inayodai malipo ( kwa ajili Mwanza Master Plan) ya hatua ya kwanza ambayo ni 15% ya fedha kama walivyokubaliana kwenye 'mkataba' (15% of the Contract value (15% x 4,483,095) inaonyesha kwamba kodi ( Local taxes ) sio tena jukumu la Mshauri mtaalam huyo, bali jukumu la Serikali ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ilieleze Bunge hili tukufu, kwa kinaga ubaga, ni lini na kwa mkataba upi jukumu la kodi lilihama kutoka kwa mshauri mtaalam kwenda kwa serikali ya Tanzania?

**Mheshimiwa Spika** Kuna taarifa pia kwamba hata hiyo fedha iliyolipwa (15%), imelipwa kabla kazi katika hatua ya kwanza haijakamilika. Makubaliano ya malipo yako katika hatua saba, katika mgawanyo wa (i) 15% (ii)15% (iii) 25% (iv) 15% (v)10% (vi) 5% (vii) 15%. Na katika kila hatua malipo yanafanyika baada kazi iliyotakiwa kufanyika katika hatua husika kukamilika. Makubaliano yanaelekeza kwamba: "*15% of the lumpsum amount shall be paid upon submission and approval of the inception report and Base Mapping*"

**Mheshimiwa Spika,** Kwa taarifa ambazo Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, malipo yaliyofanyika kwa njia ya electronic ya tarehe 15/04/2015 (Legal Receipt number 048-048VC14003705 na 048-048VC14003615) ya jumla ya shilingi 1,118,857,334 yalifanyika kabla ya kuwasilishwa na kuthibitishwa kwa inception report na base mapping! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo kuhusu jambo hili!

## 16. SERIKALI YA CCM NA MIPANGO MIJI

**Mheshimiwa Spika,** Idadi ya watu wanaoishi katika maeneo ya mijini kwa upande wa Tanzania bara imeongezeka kutoka kutoka 5.7% mwaka 1967 hadi 29.1% mwaka 2012 . Kiwango cha ukuaji wa miji kimekuwa ni kikubwa kuliko uwezo wa mamlaka husika kutoa huduma za viwanja vilivyopangwa kwa makazi na shughuli za maendeleo ya miji. Mheshimiwa Spika, katika jiji la Dar es salaam pekee linalokadiriwa kuwa na nyumba 500,000!. Tafiti[17] zinaonyesha kwamba kati ya 'hizo' nyumba 400,000 zimeendelezwa katika maeneo yasiyopangiliwa au makazi yasiyo rasmi ambayo hayajapimwa!

**Mheshimiwa Spika,** Hali kama hii ipo pia katika majiji ya Mwanza na Arusha, hali hii imesababishwa na 88% ya waendelezaji katika maeneo ya kupata viwanja kutoka katika masoko ya ardhi yasiyo rasmi!!

**Mheshimiwa Spika,** Hali hii haijatokea kwa bahati mbaya!! kwani miaka 54 baaya ya uhuru 80% ya miji haina /haijawahi kuwa 'General Planning Shemes'. Kati ya miji 148 iliyofanyiwa utafiti, miji 96 (65%) haijawahi kuandaa/kutayarisha Master Plan tokea ianzishwe, miji 52( 35%) zina Master Plan lakini ambazo zimepitwa na wakati na hazijawahi kupitiwa upya!

**Mheshimiwa Spika,** Imegundulika kuwa ni 20% ya Planning Authority zilizogundulika kuwa na 'planning scheme' lakini utekelezaji wake umekwenda kinyume kabisa na kile walichokipanga! Kwa mfano, katika jiji la Dar es salaam ambapo Master Plan ya mwaka 1979 ilipanga eneo

[17] Ripoti ya Jumla ya ukaguzi wa ufanisi na maalum kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi 2015, Ofisi ya Taifa ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali , uk.4

la Mwenge  na Mbezi kama eneo la viwanda, wakati wa utekelezaji  hali ikawa tofauti!

**Mheshimiwa Spika,** Ni dhahiri kabisa kwa usimamizi  huu duni wa mipango miji, licha ya uwepo wa sheria  ya Mipango miji  Na. 8  ya 2007 na Uanzishwaji  wa idara ya  uendelezaji  Miji ndani ya wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya makazi, Tamisemi na mamlaka ya serikali za Mitaa unaonyesha ni kwa kiwango gani  wizara ya ardhi na TAMISEMI zilivyoshindwa kusimamia kazi. Kuna ulazima mkubwa sasa , kama nchi kuangalia upya sheria, halikadhalika uwezo mamlaka za kupanga miji!

**Mheshimiwa Spika,** Katika Jiji tu la Dar es salaam tuna mamlaka za upangaji 4 tofauti za kupanga mji!!, kila  moja ina mamlaka ya kupanga halikadhalika mamlaka ya kubadilisha matumizi ya ardhi! . Haiwezekani katika karne hii kamati za mipango miji za halmashauri ambazo hazina utaalam wowote kupewa majukumu ya kitaalam ya upangaji wa mji. Lazima kuwe na mipaka!!

**Mhehsimiwa Spika,** Ni lazima mamlaka zinazotoa huduma (Tanesco, TTCL, Dawasco, Tanroad etc)  zishirikishwe katika michakato yote ya Mipango miji, katika kila hatua!kutokana na sheria za sasa kutokutambua ushirikishwaji wa vyombo vingine vinavyotoa huduma,  katika kipindi cha mwaka mmoja, serikali (Tanroads) imepoteza  shilingi  **bilioni 28.53** kama gharama za ziada  kwa malipo ya fidia na kuhamisha miundombinu. Hatuwezi kuendelea na utaratibu huu!!

## 17. ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2010-15 NA HILA ZA CCM

**Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni tumeshuhudia wanaojiita ‘watia nia’ wa

Chama Cha Mapinduzi wakitangaza nia , kwa mbwembwe nyingi na kama kawaida yao wakiwaahidi watanzania maziwa na asali! Cha kushangaza watia nia wote ambao wakiwa mbele ya Bunge lako tukufu wamekuwa mstari wa mbele kutetea kile wanachokiita 'mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya CCM', wakati wanatangaza nia huko mitaani, wanageuka ghafla wapinzani kwa kukosoa ufanisi wa utendaji kazi serikali hiyo hiyo wanayoiongoza!

**Mheshimiwa Spika,** Ili tuweze kupima ufanisi wa hiki chama…pamoja na wagombea wake ni muhimu basi tujiridhishe nini walichoahidi katika ilani na nini walichofanikiwa kutekeleza.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali hii ya CCM iliwaahidi watanzania kufanya yafuatayo:

1) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi , wenye Program 12 ambazo ni propgam ya kuimarisha TUME, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Mitu, Wanyamapori, Madini, Nishati , Miundombinu, Rasilimali maji, Utalii na uwanda/uoto asili kwa lengo la kukamilisha kazi ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi nchi-
2) Kuandaa utaratibu wa kuwawezesha wananchi wasio na ardhi katika maeneo mengine ya nchi
3) Kuziwezesha Halmashauri za miji na wilaya zote nchini kuweka na kuutumia mfumo wa kutumia teknolojia ya kompyuta katika kutoa huduma za ardhi kwa kuimarisha na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za upimaji ardhi

na kuzibadilisha kutoka mfumo uliopo sasa kuwa wa kelektroniki,

4) Kushirikiana na Halmashauri za miji na wilaya kutambua ardhi kwa ajili ya kuanzisha Hazina ya ardhi (Land bank) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi,
5) Kuzijengea uwezo Halmasauri za miji na wilaya ziweze kupima viwanja vingi na kuuza kwa wanaohitaji kwa kutumia mfuko wa mzunguko (Plot Development Revolving Fund),
6) Kuboresha utendaji kazi wa mabaraza ya wilaya ya ardhi na Nyumba 39 yaliyopo na kuanzisha mabaraza mapya 50 (wastani wa mabaraza 10 kwa kila mwaka ) kwenye wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi na nyumba -
7) Kuzijengea uwezo Halmashauri za wilaya , miji na majiji kuajiri wataalam wa kutosha wa sekta ya ardhi na kununua zana za kisasa za kupima ardhi na usanifu-

**Mheshimiwa Spika,** katika Sekta ya Nyumba, Serikali hii ya CCM iliwaahdi wananchi:

1) Kushirikiana na wakala wa Taifa wa utafiti nyumba bora na vifaa vya ujenzi (NHBRA) katika kufanya tafiti mbali mbali za vifaa vya ujenzi wa nyumba bora kwa teknolojia rahisi na gharama nafuu na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa wananchi-
2) Kuhakikisha kwamba ujenzi wa nyumba na majengo yanayotumiwa na umma unazingatia

mahitaji maalum  hususan ya watu wenye ulemavu,

3) Kuhakikisha kuwa jumla ya nyumba 15,000 (kwa wastan nyumba 3000 kila mwaka) zinajengwa na shirika la nyumba la Taifa (NHC) kwa kushirikiana na sekta binafsi-
4) Kuhimiza  uanzishwaji wa vyama vya ushirika  wa nyumba, na pia vikosi vya ujenzi wa nyumba bora  na za gharama  nafuu katika ngazi ya wilaya na Kata ili kuwezesha wananchi wa kipato cha chini kufaidika na mikopo ya nyumba -
5) Kuboresha  mazingira ya upatikanaji  wa mikopo  kwa ajili ya ujenzi  wa nyumba kwa masharti nafuu, kuwahamasisha  wananchi  kuzielewa sheria ili wazitumie kupata mikopo ya muda mrefu  kwa ajili ya kujenga  au kununua nyumba  na kuhamasisha mabenki  ya vyombo vingine  vya fedha  kutoa  mikopo ya ujenzi wa nyumba ya muda mrefu yenye riba nafuu
6) Kulielekeza Shirika la Nyumba la Taifa  kuwa mwendelezaji  ardhi mkubwa ( Master Estate Developer) na kujenga  nyumba nyingi kwa ajili ya kuuza  au kupangisha  kwa wananchi wote  na HASA  WATU WA KIPATO CHA CHINI NA CHA KATI),
7) Kutunga sheria  itakayowataka wote wanaojenga nyumba bora  na majengo mbalimbali mijini na vijijini kujenga miundombinu ya kuvuna  na kutumia maji ya mvua,
8) Kukamilisha  utungaji wa sera ya Taifa ya nyumba (Housing Policy)-
9) Kuandaa  mpango wa kampeni wa kitaifa katika kila

wilaya kuhakikisha kuwa wananchi wanajijengea nyumba bora-

10) Kuweka mazingira yatakayowezesha ujenzi wa nyumba wa gharama nafuu-

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo la Mipango Miji, Serikali ya CCM iliwaahidi watanzania:

1. Kuanzisha mji wa kisasa wa kigamboni,
2. Kulitafutia ufumbuzi tatizo la mpaka baina yetu nan chi ya Malawi katika ziwa nyasa-
3. Kutekeleza mradi kambambe wa kuweka kituo cha kupokea picha za satellite (satellite Imagery Receiving Station) kitaakachorahisisha upimaji wa ardhi yote nchini na pia kitarahisisha utayarishaji wa ramani kwa ajili ya matumizi mbali mbali.-

## 18. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kama ni kutapeliwa, wananchi wa Tanzania wametapeliwa ile mbaya na Serikali hii ya CCM kwa kuwa mambo yote waliyoahidi kwa wananchi, katika sekta ya ardhi na makazi, ahadi nyingi zimebaki kuwa ngonjera, utekelezaji HAKUNA!

**Mheshimiwa Spika,** nasema hivi kwa sababu ya propaganda na upotoshaji mkubwa unaofanywa na wanaotangaza nia ya kugombea urais kupitia CCM kwamba watawaletea wananchi neema wakati

walikuwa viongozi wakubwa Serikalini kwa miaka mingi na wakashindwa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshtushwa sana kumsikia aliyekuwa Waziri Mkuu wa Zamani Edward Lowasa akiwaambia wananchi, wakati akitangaza nia ya kugombea urais kwamba: atapambana na ufisadi iwapo atakuwa rais wakati Serikali yake ilianguka kwa kashfa kubwa ya ufisadi katika sakata la Richmond. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepigwa butwaa kumsikia pia Waziri wa Kilimo akiwahadaa wananchi kwamba akiwa rais atahakikisha kwamba jembo la mkono litawekwa kwenye makumbusho akimaanisha atawapa wananchi matrekta ili waachane na jembe la mkono. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, kwanini asiwapatie wananchi matrekta hayo sasa tena ukizingatia ndiye waziri wa Kilimo? Tulimshangaa pia aliposema atapambana na rushwa nchini wakati yeye mwenyewe alishawahi kutiwa hatiani na mahakama kwa kutoa rushwa katika uchaguzi wa ubunge na hivyo kuvuliwa ubunge na kusimamishwa asigombee nafasi yoyote kwa miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inawaonya wagombea urais wa CCM ambao walikuwa Serikalini na wakatumia nafasi zao kuwasababishia watanzania umasikini uliokithiri na sasa wanaufanya umasikini wa watanzania kama mtaji wao wa kisiasa. Tulimshangaa Mwigulu Nchemba akijigamba kwamba hakuusoma umasikini kwenye vitabu bali anaujua kwa kuzaliwa, lakini akiwa kama naibu waziri wa fedha halishauri taifa namna ya kuondokana na umasikini bali anasubiri kwanza awe rais ndio afanye hivyo. Inaingia akilini??! Hivi

mmewageuza watanzania kuwa ni mazezeta kabisa kiasi cha kuwadanganya waziwazi namna hii?

**Mheshimiwa Spika,** ni kwa msingi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawasihi wananchi, ***in a very serious note*** wapime hoja za upinzani kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne ili wajue ni nani kati ya UKAWA na CCM wanastahili kupewa ridhaa ya kuongoza Serikali ya awamu ya tano.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha

Halima James Mdee (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI**

**BUNGENI NA WAZIRI KIVULI WA ARDHI,**

**NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

8 JUNI, 2015